

Dondoo za Mkutano Mkuu wa 4 wa Mwaka uliofanyika tarehe 01 Februari 2019

Kufungua Mkutano:

Mkutano ulifunguliwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mh. Abdullah Mwinyi saa 10:15 asubuihi. Alitoa neno la ukaribisho kwa Wanahisa. Kisha akawasilishwa utaratibu wa kuendesha shughuli za mkutano kwa Wanahisa, utaratibu ambao ulijumuisha: Shughuli zitakazofanyika katika mkutano, kuhesabu wawakilishi na utaratibu wa kupiga kura.

Agenda:

Agenda ziliwasilishwa kwa Wanahisa na ndizo zilizoanza kufanyiwa kazi katika mkutano. Yaliyokuwemo katika agenda yalikuwa kama ifuatavyo: (i) Kupitia taarifa za fedha na ripoti za mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba 2017; (ii) Kuteua upya wakaguzi wa mahesabu; (iii) Kutoa taarifa ya hati fungani inayoweza kubadilishwa kuwa dhamana ya aina nyingine (convertible notes); na (iv) Kufanya mabadiliko katika katiba ya kampuni.

Shughuli Rasimi

Maazimio

1. Kupitia taarifa za fedha na ripoti za mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba 2017

Mwenyekiti aliwasilisha mabailiko ya Taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka unaoishia tarehe 31 Desemba 2017, ambayo ilikwisha wasilishwa kwa wanahisa kabla ya mkutano.

2. Kuteua upya wakaguzi wa mahesabu

Katika mkutano mkuu wa mwaka uliopita katika mwaka 2018, KPMG walichaguliwa na Wanahisa kama wakaguzi wa nje wa mahesabu ya kampuni. Mwaka huu wa 2019, Bodi ya Wakurugenzi ilipendekeza kuwachagua upya KPMG waendelea kuwa wakaguzi wa nje wa mahesabu kwa mwaka wa fedha wa 2018-2019.

Maoni: Wanahisa walihoji taarifa za kuhusu kwanini tuendelee na KPMG kwa mwaka mwingine wa fedha wa 2018-2019, ambayo ilijibiwa na Bodi.

Azimio; Wanahisa walikubaliana kuidhinisha kuteuliwa tena kwa KPMG kuendelea kuwa wakaguzi wa nje wa mahesabu ya kampuni kwa mwaka wa fedha wa 2018-2019.

3. Kuidhinisha Utolewaji wa hati fungani inayoweza kubadilishwa kuwa dhamana ya aina nyingine (convertible notes)

Mchakato ulieleza kwamba mpaka kufika kiasi cha dolla milioni \$45 zitakusanywa kutoka kwa wawekezaji wenye uwezo kupitia utolewaji wa taarifa ya hati fungani inayoweza kubadilishwa kuwa dhamana ya aina nyingine (convertible notes), itakayo badilishwa kuwa hisa katika kipindi cha miezi 3 ya awali tangu kutolewa au baada ya kuorodheshwa kwa hisa katika soko la hisa la OECD

Azimio: Wanahisa walikubaliana kuidhinisha kutolewa kwa Taarifa ya hati fungani inayoweza kubadilishwa kuwa dhamana ya aina nyingine (Convertible Notes)

4. Kuidhinisha mabadiliko katika katiba ya kampuni.

Kampuni imefanya mabadiliko fulani katika katiba yake kwaajili ya kuendana na maendeleo ya mhibiti, hususani katika kuthibitisha mtaji utokanao na hisa na Hisa za Mapendeleo. Katika ukurasa wa 7 wa Hati ya Mwongozo wa Kampuni, kulifanyika marekebisho isomeke, 'Mtaji utokanao na hisa ni TZS 150,000,000 tofauti na hati ya mwongozo wa kampuni wa hapo awali ambao mtaji utokanao na hisa ilikuwa TZS 100,000,000'.

Nakala za katiba ya kampuni iliyofanyiwa marekebisho inaweza kufanyiwa mapitio katika tovuti ya kampuni (www.swalaoilandgas.com) au kupatikana kwaajili ya kukaguliwa katika ofisi za kampuni zilizosajiliwa.

Azimio: Wanahisa walikubaliana kuidhinisha mabadiliko ya katiba ya kampuni.

Mambo mengine nje ya Agenda (AOB)"

Maoni ya jumla kutoka kwa Wanahisa.

1. Taarifa zote mpya kuhusu kampuni na mapatano yake yanapaswa kufikishwa kwa Wanahisa wa kampuni moja kwa moja, hata kama yataendelea kuwekwa katika tovuti ya kampuni, twitter na kuchapishwa katika gazeti.
2. Dondoo za mkutano mkuu wa mwaka zinapaswa kuwekwa katika tovuti na kufikishwa moja kwa moja kwa Wanahisa wa kampuni.

Kufunga Mkutano:

Mwenyekiti aliwashukuru Wanahisa kwa kuhudhuria mkutano na kwa michango yao wakati wote wa mkutano. Kisha aliwakaribisha Wanahisa kupata vinywaji na kutangaza kufunga mkutano saa 13:20 aduhuri.